# Usawiri wa Nafasi ya Mwanamke Katika Malezi: Mifano Kutoka Katika Nyimbo Teule za Bongo Fleva

Venance Gilbert Mpate
Shule ya Sekondari Chisano, Mlimba, Morogoro, Tanzania
Barua pepe: venancegilbert@gmail.com

***Ikisiri***

*Malezi ni jambo la muhimu sana katika jamii yoyote. Ni mchakato wa muda mrefu ambao huhusisha mzazi ama mlezi na mtoto katika makuzi yake. Katika jamii za Kiafrika suala la malezi hufanywa kwa kiasi kikubwa na wanawake. Makala haya yanakusudia kuchunguza usawiri wa nafasi ya wanawake katika malezi katika jamii. Makala yameongozwa na Nadharia za Ufeministi wa Kiafrika na Mwingilianomatini. Data zimepatikana kwa njia ya udurusu matini kwa kusikiliza mashairi ya nyimbo za Bongo fleva katika mtandao wa YouTube. Mbinu iliyotumika kupata nyimbo zilizotafitiwa ni usampulishaji lengwa ambapo mtafiti alisikiliza nyimbo nyingi na kupata jumla ya nyimbo kumi na saba za Bongo fleva zinazozungumzia nafasi ya mwanamke katika malezi ya watoto. Data katika makala haya zimefafanuliwa kwa njia ya maelezo. Utafiti ulibaini kuwepo mchango mkubwa unaofanywa na wanawake katika malezi kwenye jamii kama ulivyosawiriwa katika nyimbo teule za Bongo fleva. Pia utafiti ulijielekeza katika kuangalia athari hasi za kukosekana kwa nafasi ya mama[2] katika malezi na makuzi ya mtoto.*

**Manenomsingi**: Bongo fleva, malezi, usawiri.

## 1.0 Utangulizi

Bongo fleva ni utanzu wa ushairi simulizi ambao ulianza miaka ya 1980 nchini Tanzania (Lucas, 2022). Dhana ya muziki wa Bongo fleva imefasiliwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwa wataalamu hao ni (Omari, 2009) anayedai kwamba muziki huu umetokana na muziki wa kufoka foka maarufu kama Hip Hop. Lupogo (2019) anadai kwamba Bongo fleva ni kapu linalojumuisha kila aina ya muziki unaopatikana nchini Tanzania na kwa ufafanuzi wake anadai kwamba kapu hilo huhusisha miziki ya Taarab, Zuku, Hip Hop, R&B, Rege, Injili, Singeli na Nyimbo za Asili zinazoimbwa nchini Tanzania. Kutokana na maelezo haya ya Lupogo ni wazi kwamba nyimbo zote zinazoimbwa nchini zinaingia katika kundi la Bongo fleva. Kasiga (2021) anadai kwamba kukua kwa muziki huu kumeleta mitindo mbalimbali yenye asili ya Tanzania na kigeni. Hii ndiyo sababu muziki huu una vionjo mbalimbali kutoka sehemu nyingi za dunia

[2] Kwa muktadha wa makala haya neno mama laweza kutumika kama kisawe mwanamke.

kama Nigeria, Afrika Kusini, Kongo, Marekani, Uingereza na kwingineko. Kwa ufafanuzi huu ni dhahiri kwamba muziki huu hauna asili moja.

Dhana ya malezi imefafanuliwa kwa maana mbalimbali na vyanzo tofautitofauti. TUKI (2019) wanafasili malezi kama njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kutarajiwa kufuata tabia na mwenendo unaostahiki. Kituo cha Uangalizi cha Al-Azhar (2021) wanafasili malezi kama zoezi la kuunda mwenendo na tabia ya mtu kuanzia utotoni kwa mujibu wa vidhibati na vyanzo maalumu kidini, kijamii, kiuchumi na kifikra.

Mwananchi (2018) wanafafanua malezi kama mchakato wa maandalizi ya mtoto utakaomwezesha kukua, kukubalika na kushiriki katika shughuli za kijamii na kitamaduni kwa kumlinda, kumjamiisha na kumpatia mahitaji na huduma za msingi. Pia wanasisitiza kuwepo mipango toka kwa wazazi ili kufanikisha mchakato huo.

Sema Tanzania (2023) wanabainisha kuwa hakuna mfumo maalum katika malezi ya watoto ila familia na jamii nzima ina jukumu kubwa katika malezi ya watoto, likiwemo kuwalea kwa mapenzi makubwa. Sema Tanzania (wameshatajwa) wanataja mambo sita muhimu katika malezi ya watoto ambayo ni upendo wa dhati, mfumo maalum wa maisha ya malezi, kumwelewa motto, kuwa mfano mzuri wa kuigwa, changamoto za utoto na kushirikishwa katika familia.

Chama Cha Mapinduzi (1987) kimewahi kuzungumzia maana tano za malezi katika Sera ya Malezi ya Taifa kwa Watoto na Vijana wakati ambao nchi ilikuwa katika mfumo wa chama kimoja cha siasa. Katika muktadha wa makala haya fasili ya tano ndiyo ilionekana kufaa zaidi. Fasili hiyo inadokeza kwamba malezi ni shughuli zote za kumtunza mtoto, kumfundisha au kumpa maelekezo yatakayomsaidia katika kukuza vyema mwili wake, akili yake, maono yake, vipaji vyake, utashi na uhodari wake ili atakapofikia utu uzima awe mtu mwenye manufaa kwake yeye mwenyewe na kwa taifa lake.

Kwa mujibu wa fasili zilizozungumzwa hapo juu makala haya yanafasili malezi kama utaratibu na namna ya kumtunza na kumlinda mtoto, tangu akiwa tumboni kwa mama yake hadi anapozaliwa na kujitambua. Katika kipindi hicho cha malezi wazazi ama walezi huwa taa ya mtoto katika mambo yote. Huwajibika kuhakikisha mtoto anapata mwongozo sahihi, mahitaji ya

muhimu katika maisha na kumfunza tabia njema na kumtofautishia mabaya ili aje kuwa mtu bora katika maisha yake na jamii yake.

## 2.0 Nadharia za Utafiti

Makala haya yameongozwa na Nadharia za Ufeministi wa Kiafrika na Mwingilianomatini. Mkabala huu wa uhakiki hujaribu kuelezea changamoto wanazokutana nazo wanawake wa Kiafrika, kinachozisababisha changamoto hizo na jinsi ya kuepukana nazo. Filomina Steady raia wa Sierra Leone ndiye anatajwa kuwa mwasisi wa mkabala huu wa uhakiki. Steady anabainisha kuwa dhuluma ambazo wanakabiliana nazo wanawake wa Kiafrika ni kama vile kutokuwa na uwezo wa kuchagua kuwa mzazi au mke wa mtu, ukeketaji wa wanawake, unyamavu wa kulazimishwa, unyanyasaji kutoka nje, urithi wa mila na desturi, rangi yake mwenyewe na vilevile kuonewa kwa wanawake tasa (Steady, 1981).

Steady (keshatajwa) anaeleza kuwa Ufeministi wa Kiafrika katika fasihi unafaa kuchunguza hali za kijamii na kiutamaduni zinazochangia ukandamizwaji wa wanawake wa Kiafrika. Katika kujadili usawiri wa nafasi ya mwanamke katika malezi, makala haya yamekita mizizi katika mihimili ifuatayo:

i) Mwanamke wa Kiafrika anaweza kujitegemea na kuishi bila ya kudhulumiwa;
ii) Mwanamke wa Kiafrika ana nafasi kubwa katika ujenzi wa jamii ambayo yeye ni mshiriki;
iii) Mwanamke wa Kiafrika anaweza kuwa shujaa;
iv) Uhalisia wa wanawake wa Kiafrika unadhihirika katika fasihi ya Kiswahili.

Makala haya pia yatachunguza umuhimu wa mwanamke katika malezi ya watoto kwenye jamii. Katika kufanikisha jambo hili nyimbo kumi na saba zimerejelewa ili kuonesha ushujaa wa mwanamke na namna anavyotegemewa. Nyimbo zinazorejelewa zinaonesha ushujaa wa mwanamke na namna anavyotegemewa. Kwa hivyo mihimili hii ndiyo itasaidia katika uchambuzi wa matini lengwa.

Kohrs-Amissah (2002) anaeleza kwamba Ufeministi wa Kiafrika haujihusishi tu na kusuluhisha migongano kati ya wanawake na wanaume kwani kuliondoa tatizo moja hakutasuluhisha

matatizo yanayowasibu wanawake wa Kiafrika. Hata usawa ukiwapo kati ya wanaume na wanawake matatizo kama vile athari za kikoloni na ubaguzi bado yatakuwepo. Nadharia hii pia huchunguza asasi zilizo katika jamii za Kiafrika ambazo zinamthamini mwanamke na kupuuza zile zinazowaletea madhara. Aidha, makala haya pia yataonesha bayana nafasi ya mwanamke katika malezi pale yanapokosekana.

Nadharia nyingine ni Mwingilianomatini. Mulokozi (2017) anaeleza kwamba Nadharia ya Mwingilianomatini iliasisiwa na Julia Kristeva. Huyu ni mwanasemiotiki wa Kifaransa aliyeibua Nadharia hii kutokana na mawazo ya nadharia za Ki-Bakhtini hasa Nadharia ya Usemezano au Daiyolojia. Kristeva (1980) anaeleza kwamba mwingilianomatini ni uumbaji wa maana ya matini kwa kutegemea matini nyingine. Wamitila (2003) na Kyarendwa (2014) wanaeleza kuwa Nadharia ya Usemezano hushadidia kwamba kila matini huwa na athari ya matini zilizotangulia au zitakazofuata; maandiko yaliyotangulia huchochea maandiko ya baadaye. Kyarendwa (keshatajwa) anafafanua kwamba athari ya kazi moja ya fasihi huweza kuonekena katika kazi nyingine licha ya kuandikwa na waandishi tofauti wenye uzoefu tofauti na hata kutoka katika jamii tofauti. Allen (2000) anaifafanua dhana ya Mwingilianomatini kama uhusiano, muunganiko na kutegemeana kwa kazi za fasihi katika utamaduni wa baada ya usasa. Waitifaki wa nadharia hii wanaamini kwamba ni vigumu kwa jamii ya sasa kuibua kazi mpya ya fasihi ambayo haijawahi kuzungumziwa hapo awali. Mwingilianomatini unaweza kutazamwa katika vipengele vya mtindo, maudhui, wahusika, motifu na dhamira (Wamitila, 2008). Kwa hivyo katika makala haya matini moja inaweza kufanana na nyingine katika vipengele hivyo vilivyotajwa, hii ni sababu iliyopelekea kuchagua nadharia tajwa.

**3.0 Mbinu za Utafiti**

Data katika makala haya zimepatikana kwa usampulishaji lengwa. Mwandishi wa makala haya alisikiliza nyimbo za Bongo fleva na kupata sampuli ya nyimbo kumi na saba ambazo ziliendana na utafiti huu. Data zote zimechanganuliwa na kufafanuliwa kwa njia ya maelezo. Jedwali lifuatalo linaonesha nyimbo zilizotafitiwa.

Jedwali la Kwanza: Orodha ya Nyimbo Zilizotafitiwa.

| Na. | Wimbo | Mwanamuziki |
|---|---|---|
| 1. | Akilia Mama | Yvonne Chakachaka ft[3] Ali Kiba |
| 2. | Hawajui | Vanessa Mdee |
| 3. | Mama | B2K |
| 4. | Mama | Banana Zorro &[4] Peter Msechu |
| 5. | Mama | Bashary |
| 6. | Mama | Ben Pol & Goodluck Gozbert |
| 7. | Mama | Harmonize |
| 8. | Mama | Kasi Simela |
| 9. | Mama | Kayumba |
| 10. | Mama | Rayvanny |
| 11. | Mama | Yamoto Band |
| 12. | Mama Yangu | Banana Zorro |
| 13. | Mbagala | Diamond Platnumz |
| 14. | Mkuki Moyoni | Afande Sele |
| 15. | Nani Kama Mama | Christian Bella ft Ommy Dimpoz |
| 16. | Nitakupa Nini | King Crazy GK |
| 17. | Wanawake na Maendeleo | Vick Kamata |

## 4.0 Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii imegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni usawiri wa nafasi ya mwanamke katika malezi na athari hasi za kukosekana kwa mwanamke katika malezi ya mtoto.

### 4.1 Usawiri wa Nafasi ya Mwanamke katika Malezi

Katika sehemu hii utafiti umeonesha mambo mbalimbali anayofanya mwanamke katika malezi ya watoto kwenye jamii. Utafiti umebaini mwanamke kupewa uhusika wa kishujaa, hadhi ya juu, tegemeo katika malezi na mambo mengine kama jinsi Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unavyotaka kumtazama mwanamke. Maelezo yafuatayo ni ufafanuzi wa nafasi ya mwanamke katika malezi ya watoto kama alivyosawiriwa katika nyimbo teule za Bongo fleva.

[3] ft ni kifupisho cha neno la kiingereza 'featuring' linalotumiwa kwenye muziki kuonesha mwanaumuziki anayetajwa mbele ameshirikishwa katika wimbo tajwa.

[4] Alama & hutumika kuonesha ushirikiano wa wasanii katika wimbo husika. Wakati mwingine herufi X hutumika badala ya alama hiyo.

**4.1.1 Mvumilivu na asiyechoka**

Mwanamke amesawiriwa kama mtu mvumilivu katika mchakato wa malezi. Neno mvumilivu limetokana na nomino uvumilivu ambayo imefasiliwa na TUKI (2019) kama hali ya kustahmili machungu. Nomino hii inavyo visawe vingine kama ustahamilivu na subira ambavyo vyote vina maana sawa. Ni sawa kumsawiri mwanamke kama mwenye subira na mstahamilivu. Katika makala haya uvumilivu wa mwanmke unazungumziwa katika nyanja za mambo yote anayopitia tangu akiwa mjamzito, wakati wa kujifungua na kulea mtoto hadi mtoto ajitambue. Katika mtazamo wa kawaida mambo haya yanaweza kuonekana kama majukumu ya kijinsia lakini kimsingi ni majukumu makubwa na yenye kuhitaji ustahamilivu wa hali ya juu. Uhalisia wa maisha ya Kiafrika umezungungukwa na mambo mengi katika malezi, mathalani, mwanamke anaweza kuwa analea watoto wadogo wenye umri tofauti chini ya miaka kumi na wakati huo huo akawa ni mjaumzito, kama si uvumilivu mambo yote hayo yasingefanyika. Katika nyimbo za Bongo fleva mwanamke ameoneshwa kama mvumilivu kwa yote yaliyotajwa hapo juu. Mwanamuziki Banana Zorro katika wimbo wake Mama Yangu anathibitisha hili anaposema

*Umenilea tangu nazaliwa*

*Haukuchoshoshwa na wangu usumbufu*

*Muda wako mwingi mama uliutumia kwa ajili yangu*

Mishororo hii inadhihirisha uvumilivu wa mwanamke katika malezi ya mwanaye. Msanii anagusia namna ambavyo mama yake hakuchoshwa na tabia zake za usumbufu alipokuwa mtoto. Ni dhahiri kwamba watoto huwa na usumbufu mwingi katika malezi kwa wazazi ama walezi na jamii nzima, hii ni kwa vile huwa na tabia za udadisi wa mambo mengi wanayotaka kuyapatia majibu. Aidha ukorofi, kiburi, maradhi na mengineyo ni miongoni mwa usumbufu wa watoto.

Fauka ya hayo mwanamuziki Kayumba katika wimbo wake Mama anasema

*Walivumilia leba walipotupata*

*Wapo walokataliwa (mama)*

*Na milango kufungiwa (mama)*

*Nyumbani kutimuliwa (mama)*

*Na mali kudhulumiwa (mama)*

Mishororo hii inaonesha uvumilivu wa mwanamke katika mambo mengi katika malezi ya watoto. Kwanza mwanamuziki anaeleza uvumilivu wa uchungu ambao wanawake huuhisi wanapokuwa wanataka kujifungua. Pili anaonesha uvumilivu wa mwanamke hasa waliotelekezwa na watoto kwa kukataliwa na wazazi wenza. Tatu anasawiri uvumilivu wa mwanamke baada ya kufukuzwa nyumbani na hata wajane ambao hudhulumiwa mali baada ya kufiwa na wenza wao. Katika hayo yote wanawake huvumilia na kulea watoto wao hata wakakua wakiwapatia mahitaji yote ya msingi.

Mwanamuziki Ben Pol katika wimbo wake Mama pia anaimba kuhusu uvumilivu wa mwanamke anaposema

*Miezi tisa tumboni sijui lolote ila Mama kabisa ulininingojea*

*Ukashona na sare kusubiri nianze shule*

Mishororo hii inadhihirisha uvumilivu wa mwanamke katika malezi tangu awapo mjamzito na uvumilivu wake kwa mtoto hadi atakapoanza shule. Pia mwanamuziki Christian Bella katika wimbo wake Nani Kama Mama anaposema

*Oh yah nani kama mama, heshima kwa mama*

*Yale mateso ulinibeba miezi mitisa tumboni mwako*

*Pole sana mama, nikupe nini?*

*Uliteseka siku ya kunitoa duniani*

Mishororo hii pia inaonesha uvumilivu wa mwanamke tangu awapo mjamzito hadi kujifungua. Mwanamuziki anazungumzia mateso apitiayo mwanamke wakati wa kujifungua akitaja maumivu ya uchungu. Ni dhahiri kuwa mwanamke ni mvumilivu katika mchakato wa malezi ya watoto. Yamoto Band katika wimbo uitwao Mama pia wamesawiri hali ya mwanamke kutochoka wanaposema

*Muda mwingine najisaidia hauchoki kufua*

*Muda mwingine nakuudhi pia haukunichukia*

Mishororo hii pia inadhihirisha uvumilivu wa mwanamke katika malezi hasa katika hali na tabia za mwanawe. Hayo yote na mengine mengi yanaonesha namna mwanamke anavyovumilia changamoto kadha wa kadha kabla ya kujifungua na baada ya kujifungua.

#### 4.1.2 Mwenye kujali

Mwanamke ameoneshwa kama mtu mwenye kujali kwa mambo anayofanya katika mchakato mzima wa malezi. Nyimbo nyingi ambazo zimechunguzwa katika makala haya zimeimbwa na wanaume. Yawezekana kila mmoja alipata nafasi ya kushuhudia yote aliyoyaimba ndiyo ikawa chachu ya utunzi huo. Kwa mfano, mwanamuziki aitwaye Goodluck Gozbert, katika wimbo wake uitwao *Mama* aliouimba na Ben Pol, anasema:

*Sijasahau sadaka zako kutoka moyoni*

*Uliponipa wakati Mama yangu hauna*

Mishororo hii inadhihirisha tabia ya kujali aliyonayo mwanamke kwa mtoto wake. Mwanamke huyo anatajwa kujinyima na kuhakikisha anakidhi mahitaji ya mwanawe. Vilevile, mwanamuziki Beka Flavour katika wimbo Mama ulioimbwa na kundi la Yamoto Band anathibitisha tabia ya mwanamke kujali anaposema

*Usiku ukifika ulikuwa ukiforce mapema mi nilale*

*Hutaki nikeshe wakati kesho inabidi niende shule*

Mishororo hii inamtaja mwanamke kama mtu anayejali kwa kuzingatia elimu ya mwanawe. Mama anayejali humkumbusha mwanawe kulala mapema usiku ili asipitiwe na usingizi asubuhi akachelewa shule. Christian Bella pia anadhihirisha tabia ya mwanamke kujali katika wimbo wake uitwao Nani Kama Mama anaposema

*Nikikumbuka zamani nilipokuwa mutoto*

*Nikilia usiku mama lazima utakesha na mimi*

*Huwezi kukubali niwe macho usiku nawe ufumbe macho yako*

Mishororo hii ni mwendelezo wa udhihirisho kuwa mwanamke ni mtu anayejali. Hapa amezungumziwa kama mtu anayekesha na mtoto kama hajalala hasa nyakati ambazo watoto

wadogo husumbua usiku. Pia mwanamuziki King Crazy GK katika wimbo wake Nitakupa Nini anasawiri kujali kwa wanawake anaposema

*Mwaka tisini na tatu nakumbuka niliugua*

*Nikiwa shule boarding kule Mbeya*

*Nilipozidiwa Muhimbili wakanihamishia*

*Miezi mitatu kitandani sikuweza kutembea*

*Kula ulikuacha kitanda ukakikimbia*

*Ukalala chini upate kunihudumia*

Mishororo hiyo pia inasawiri tabia ya kujali aliyonayo mwanamke katika malezi. Mwanamuziki anaelezea mama yake alivyomjali alipougua wakati alipokuwa shuleni na kueleza namna mama yake aliacha mambo yake yote na kutenga muda wa kumuuguza. Anasema katika kipindi cha miezi mitatu aliyougua na kulala kitandani pasi na kutembea mama yake alikuwepo pembeni yake hata akasahau kurudi nyumbani. Huu ni udhihirisho wa tabia ya kujali aliyo nayo mwanamke katika malezi.

### 4.1.3 Mlinzi thabiti

TUKI (2019) wanafasili neno mlinzi kama mtu ambaye kazi yake ni kuangalia usalama wa mahali fulani; mtu mwenye kulinda kinachotakiwa kuhifahiwa na kutunzwa. Kwa muktadha wa utafiti huu mlinzi ni mtu ambaye anaangalia usalama wa mtoto, kumlinda dhidi ya hatari na kumtunza. Nyimbo za Bongo fleva zimesawiri uimara wa mwanamke katika kumlinda mtoto kwa ulinzi thabiti. Katika malezi ya mtoto kumlinda ni kuhakikisha anakuwa salama kwa kumwepusha dhidi ya hatari, magonjwa, kumtunza kwa mahitaji ya muhimu na mengine yanayohusiana na malezi. Mwanamuziki Kayumba anathibitisha ulinzi wa mwanamke kwa mwanawe katika wimbo wake Mama anaposema

*Moyo unaniwaka moto*

*Jinsi ulivyonihandle usiku haulali*

*Vihoma homa baridi kali*

*Ukanilinda kama mboni yako*

Hapa Kayumba anadhihirisha ulinzi wa mwanamke kwa mtoto wake dhidi ya magonjwa kama vile homa na hata hali za hewa kama baridi kali. Anaonesha mwanamke alivyomtunza mwanawe kwa umakini kama mboni yake. Katika rejea ya mwisho neno mboni linaweza kufasiliwa kama ishara ya umakini aliokuwa nao mama huyo. Uthibitisho mwingine tunaweza kuupata katika hoja namba 4.1.2 hapo juu namna mwanamuziki King Crazy GK anavyoelezea namna mama yake alivyomlinda alipokuwa anaumwa.

Halikadhalika mwanamuziki Beka Flavour mmoja wa wasanii waliowahi kuwa katika kundi la muziki la Yamoto Band, katika wimbo wao uitwao Mama anadhihirisha ulinzi wa mwanamke kwa mwanawe anaposema

*Mama uligombana na majirani sababu mimi*

*Kunitetea hata kama kosa nafanya mimi*

Mishororo hii inasawiri ulinzi wa Mama kwa mwanawe. Mwanamuziki Beka Flavour anaonesha namna mama yake alivyomlinda hata ilipobidi kugombana na majirani kwa ajili yake. Ingawa kimalezi jambo la mzazi kugombana na majirani pale mtoto anapokosea si sahihi kwa kuwa linamtengeneza mtoto kuwa mkorofi kitabia na kupelekea kuwa kikwazo kwa wengine bado data hii ni muhimu katika utafiti huu. Umuhimu wa data hiyo katika makala haya ni namna mama au mwanamke anavyoonekana kumlinda mwanaye.

### 4.1.4 Mtu mwenye mtazamo chanya

Mwanamke amesawiriwa kama mtu mwenye mtazamo chanya katika nyimbo za Bongo fleva. Mtazamo chanya ni kufikiria mambo mema na yenye heri kila wakati bila kuyumbishwa na mawazo ya watu wengine. AliKiba katika wimbo Akilia Mama alioshirikishwa na mwanamuziki Yvonne Chakachaka[5] anathibitisha hoja hii anaposema

*Akili ya mama mawazo ya mama yanafanya kazi*

[5] Yvonne Chakachaka ni mwanamuziki wa Afrika Kusini. Wimbo huu umewekwa katika kundi hili kutokana na kumshirikisha AliKiba ambaye ni mwanamuziki wa Bongo fleva. Hata hivyo wimbo huu unafanana na nyimbo za Bongofleva kutokana na kuwa na nduni zote bainifu.

Mshororo huu unadhihirisha uchanya wa mawazo ya mwanamke katika malezi. Ni dhahiri akili ya mwanamke huwaza mambo mengi sana kila siku, mathalani, atawaza mtoto kuvaa nini, kupika, kufua, kufanya usafi wa nyumba, kuwaza mlo wa kutwa wa siku nyumbani, wakati mwingine hata kutembelea ndugu, jamaa na marafiki, kuchota maji, kufikiria kesho ya watoto na mengine mengi. Hayo yote yanadhihirisha uchanya wa mawazo ya mwanamke katika malezi. Aidha, Ben Pol katika wimbo wake uitwao Mama anadhihirisha uchanya wa mawazo ya mwanamke anaposema

*Ukashona na sare kusubiri nianze shule*

*Wakasema chizi yule si angengoja akue*

Mishororo hii inaonesha uchanya wa mawazo ya mwanamke katika malezi. Fasili ya mashairi haya yaweza kumaanisha kufikiria kesho njema ya mtoto kupitia elimu. Ni dhahiri kwamba elimu ndilo jambo la muhimu katika dunia ya sasa. Katika maisha elimu humtambulisha mtu kwenye ulimwengu wa kujua kusoma na kuandika na huo ni mwanzo wa kutoa ujinga katika vichwa vya watu.

**4.1.5 Mtabiri**

Mwanamke amesawiriwa kama mtabiri wa mambo yajayo. Kwa mujibu wa TUKI (2019) kutabiri ni kueleza au kutoa habari ya mambo yatakayotokea kwa kutumia ujuzi au kwa kutafsiri ndoto. Nyimbo za Bongo fleva zimemsawiri mwanamke kama mtabiri wa mambo yatayotokea kwa wanawe kupitia uzoefu. Hii ni kumuandaa mtoto na mambo ambayo yanaweza kumtokea baadaye ukubwani. Katika wimbo wa Mama ulioimbwa na Yamoto Band, mwanamuziki Mbosso anaeleza

*Mama oo mama ee mwanao nimekua ee najionea ee*

*Mama oo mama ee mwanao najionea ee yale ya dunia ee*

*Uliyoniambia ee, umenifunza kuna kovu na ndui*

*Kuna masika na vuli, ndimu sio chungwa*

*Kuna maziwa na tui, pia simba na chui*

Katika mishororo hii mwanamuziki anaeleza mambo aliyoambiwa na mama yake alipokuwa mdogo. Mambo hayo aliyoambiwa yamekuja kumtokea baadaye ndiyo maana anasema kwamba anajionea ya dunia aliyombiwa. Mama yake huyo alimwambia kutakuwa na masika na vuli akimaanisha kwamba katika utafutaji wake upo wakati atafanikiwa sana na kuna wakati atafanikiwa kwa kiasi. Pia kovu na ndui kumaanisha yapo mambo ambayo yatamjeruhi na kumuachia alama na kumbukumbu mbaya ilihali mengine yataacha makovu yenye kumbukumbu nzuri. Maziwa na tui kumaanisha vitu halisi na visivyo halisi. Ndimu sio chungwa na simba na chui kumaanisha si watu wote atakaokutana nao katika maisha watakuwa rafiki zake ama wema kwake. Wengine watakua katika maisha yake ila ni maadui.

Fauka ya hayo, mwanamuziki Ommy Dimpoz katika wimbo uitwao Nani Kama Mama alioshirikishwa na Christian Bella anadhihirisha utabiri uliofanywa na mwanamke anaposema

*Matatizo ya dunia ee kweli ninayapitia ee*

*Yale uliyoniusia ee ya kweli mama ee*

Mishororo hii inadhihirisha kwamba mwanamke ambaye ni mama yake aliwahi kumtabiria kukutana na matatizo katika maisha yake siku zijazo hasa ukubwani. Mwanamuziki anakiri kweli kuyaona yote yaliyotabiriwa na mama yake alipokuwa mdogo.

### 4.1.6 Mwenye hekima na busara

Hekima ni maarifa yaliyopatikana kutokana na uzoefu wa muda mrefu ilhali busara ni akili na werevu wa kuweza kufikiria na kuamua kutenda jambo linalofaa (TUKI, 2019). Nyimbo za Bongo fleva zimemsawiri mwanamke kama mtu mwenye hekima na busara. Diamond Platnumz katika wimbo wake uitwao Mbagala anathibitisha hekima na busara za mwanamke anaposema

*Busara na upole na hekima niliyorithi kutoka kwa mama yangu…*

Mshororo huu unadhihirisha hekima na busara alizonazo mwanamke hata kijana wake akazirithi. Iko wazi kwamba si kila jambo mtoto hufunzwa na mzazi wake kwa kuambiwa moja kwa moja. Yapo mengine ambayo watoto hujifunza kutokana na namna mzazi anavyotenda, hiki ndicho Diamond Platnumz anachokimaanisha hapa. Halikadhalika mwanamuziki Kayumba katika wimbo wake unaoitwa Mama anasema

*Maneno yako na busara zako zinazunguka kichwani mwangu*

Mwanamuziki anadhihirisha busara alizonazo nazo mwanamke. Ingawa katika kujadili nafasi ya mwanamke katika jamii amekuwa akidunishwa kwa matendo mengi yasiyofaa, Kayumba anamwinua mwanamke kuwa mwenye busara ambazo anazikumbuka kichwani mwake mara kwa mara. Ni dhahiri kwamba kuna namna busara hizo za mama yake humsaidia katika maisha yake ya kila siku. Ommy Dimpoz pia katika wimbo uitwao Nani Kama Mama alioshirikishwa na Christian Bella anathibitisha hoja hii anaposema

*Tabia na heshima ee, busara na hekima ee*

*Ulinifundisha vyema ee*

Sauti katika wimbo huu inadhihirisha mwanamke kuwa na hekima na busara ambavyo pia alimfunza mwanawe. Sanjari na hayo alifunza heshima na tabia njema. Matini zote hizi zinathibitisha kwamba mwanamke wa Kiafrika ana nafasi kubwa katika ujenzi wa jamii ambayo yeye ni mshiriki kama ilivyodokezwa katika mhimili mmojawapo katika Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika.

### 4.1.7 Tegemeo

Mwanamke amesawiriwa kama tegemeo katika jamii. Ni vyema kutofautisha tegemeo na tegemezi: kwamba tegemeo ni namna ya kutegemewa katika jambo fulani wakati tegemezi ni namna ya kumtegemea mtu. Ni dhahiri kwamba hoja hii inafungamana na mihimili yote hapo iliyoainishwa katika Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Mwanamuziki Banana Zorro katika wimbo uitwao Mama anadhirisha mwanamke kutegemewa anaposema

*Licha ya vituko vyangu, mambo yote mabaya yangu bado uko karibu yangu wewe*

*Kuna wakati sirudi nyumbani na starehe za mjini*

*Wawakumbatia watoto wawaonesha picha zangu mimi*

*Wewe wakipekee mpenzi wangu, wewe ndiyo mama yangu*

*Sina hata pakugeukia, pakukimbilia, unanivumilia sana oo mama*

*Sijui hata wanangu shuleni wanavaa vitu gani*

*Sijui hata wanangu kule wanakulaga nini*

Mishororo hii inaonesha namna mwanamke anavyotegemewa katika malezi kwenye jamii sio tu kwa watoto wake bali hata kwa mumewe. Katika data hapo juu sauti ya mwimbaji ni mwanaume aliyelowea katika starehe na kuwa mtoro katika malezi. Licha ya yote hayo mwanamke amesimama imara kwa wanawe kwa kuwapatia mahitaji yote watakayo. Pia sauti hiyo inakiri kwamba mke wake ni tegemeo lake na hakuna mtu mwingine. Mwanamuziki Vick Kamata pia anadhihirisha namna mwanamke anavyotegemewa anaposema

*Tangu enzi za mababu yaeleweka wazi*

*Mama ndiye mlezi mkuu wa jamii*

Mishororo hii inaonesha umuhimu wa mwanamke katika malezi si tu kwa watoto bali jamii nzima. Mwanamke amekuwa akitegemewa katika kuilea jamii tangu enzi za mababu kwa kufanya shughuli za muhimu nyumbani kama vile usafi, malezi, kupika, kuosha vyombo na kuteka maji pamoja na mengine mengi. Inapotokea mwanamke akakosekana katika majukumu tajwa na mengine mengi basi wanaume wengi hulalamika na kutambua nafasi ya mwanamke.

Pia Banana Zorro katika wimbo wake uitwao Mama Yangu anadhihirisha mwanamke kuwa tegemeo anaposema

*Mama yangu wewe ni nguzo maishani mwangu*

*Taa imulikayo mbele yangu*

*Mawazo yako mama yanaongoza maisha yangu*

Mishororo hii inadhihirisha namna sauti inayoimba inavyothibitisha kumtegemea mwanamke. Neno nguzo limetumika kama ishara kumaanisha tegemeo la muhimu sana, vivyo hivyo neno taa ambayo ni ishara ya kuangaza. Hii ina maana kwamba mwanamke anategemewa kuangaza maisha ya watu katika jamii kupitia mawazo yake na ushauri wake.

### 4.1.8 Mwenye kufunza tabia njema na mwenye hadhi ya juu

Mwanamke katika nyimbo teule amesawiriwa kama mtu anayefunza tabia njema watoto na kukemea zile zisizofaa. Yvonne Chakachaka katika wimbo wake Akilia Mama anathibitisha hilo anaposema

*Nimemfunza kutunza heshima na nzuri tabia*

*Hata ukimuoa hutojutia*

Mishororo hii inadhihirisha tabia njema aliyonayo mwanamke kwa kumfunza binti yake kuwa na heshima na pia kumuandaa kuja kuwa mke bora na pengine mama bora kwa wanawe. Pia mwanamuziki Harmonize katika wimbo wake uitwao Mama anasema

*Ulinisihi vya kudhulumu ni makosa kwa Rabana*

Mshororo huu pia unadhihirisha tabia ya mwanamke kukemea tabia ambazo hazifai kwa mwanawe kuwa nazo. Halikadhalika mwanamuziki Vanessa Mdee katika wimbo wake uitwao Hawajui anathibitisha kufunzwa na mama anaposema

*Hamjui tu nyie alichonifunza mama*

*Na ndiyo maana hamuishi kutukana*

Ni dhahiri kwamba mwanamke alimfunza mwanawe kutojibizana na watu wanaomsema vibaya hasa wale wanaomtukana na hata kumsengenya. Pia mwanamuziki Banana Zorro katika wimbo wake uitwao Mama Yangu anasema

*Nikikumbuka mema ulonifundisha*

*Nashindwa hata jinsi ya kuelezea*

Hoja hii inazidi kusisitiza kuhusu tabia ya mwanamke kumfunza mema mwanawe ili aje kuwa mtu mwema na wakutegemewa katika jamii. Fauka ya hayo mwanamke amesawiriwa kama mwenye hadhi ya juu sana. Hili linathibitishwa na uwepo mashairi yanayomuenzi mwanamke katika hadi ya juu sana katika wimbo wa mwanamuziki Goodluck Gozbert uitwao Mama anaposema

*Ukitoa Mungu, Mbunge ni wewe ni wewe*

*Waziri ni wewe ni wewe*

*Rais ni wewe ni wewe Mama*

*Kila kitu ni wewe ni wewe*

Mishororo hii inaonesha hadhi aliyopewa mwanamke na mtunzi wa wimbo huu. Anampa hadhi ya Ubunge, Uwaziri na Urais ambazo ni hadhi zenye heshima ya juu katika jamii na mifumo ya tawala za kisiasa. Pia anahitimisha kwa kumpa heshima ya kila hadhi iliyopo hapa duniani kwa kusema kila kitu ni hadhi ya mwanamke. Halikadhalika mwanamuziki Christian Bella katika wimbo wake uitwao Mama anasema

*Malezi ya mama, elimu ya mama*

*Haina ada wala cheti ila ni zaidi ya elimu ya Chuo Kikuu…*

*…thamani ya malezi yako siwezi kuyalipa*

Mishororo hii inaonesha hadhi aliyonayo mwanamke sanjari na hadhi ya malezi anayotoa. Mtunzi anamsifu mwanamke kwa kusema elimu yake kupitia malezi aliyompa ni zaidi ya elimu ya chuo kikuu. Katika mantiki ya kawaida, elimu ya Chuo Kikuu ndiyo yenye hadhi ya juu na ya kuheshimika sana katika jamii. Mtunzi anapoyasifu malezi ya mwanamke kwamba yanazidi elimu ya chuo kikuu ni sawa na kumsifu mwanamke kuwa wa hadhi ya juu kwa vile yeye ndiye mfundishaji wa elimu hiyo. Vilevile anayapa thamani malezi ya mwanamke kwa kusema hawezi kuyalipa kwa vile thamani yake haipimiki kwa pesa ama kitu chochote, wazo linaloungwa mkono na mwanamuziki Kayumba pia katika wimbo wake uitwao Mama anaposema

*Hata kama nikisema nikushukuru*

*Pesa na mavogue bado*

*Hata nijenge nyumba mithili ya Ikulu*

*Kufika upendo wako bado*

Mishororo hii inadhihirisha hadhi ya juu aliyonayo mwanamke katika jamii. Mtunzi anashindwa kulinganisha thamani ya malezi ya mwanamke kwa gari za kifahari kama *Vogue*, pesa na hata nyumba za kifahari kama Ikulu. Hapana shaka kwamba Ikulu ni nyumba yenye hesima na hadhi ya juu katika taifa lolote. Mtunzi anaposema hata ajenge nyumba mithili ya Ikulu haiwezi kufikia thamani ya malezi ya mama yake ni udhihirisho kwamba thamani ya malezi ya mwanamke aliyoionesha kupitia upendo wake ni ya hadhi ya juu sana.

**4.2 Athari hasi za kukosekana mama katika malezi**

Sehemu hii inajadili kuhusu athari hasi za kukosekana kwa mwanamke kama mama mzazi wa mtoto katika malezi. Kabla ya kujadili athari hasi za kukosekana kwa mwanamke katika malezi ni muhimu kufahamu maana ya neno athari kama lilivyotumika katika utafiti huu. Kwa mujibu wa TUKI (2019) athari ni matokeo au alama inayobakia kwa muda baada ya mtu au kitu kufikwa na jambo fulani. Katika utafiti huu athari hasi zitachunguzwa ama madhara ya kukosekana kwa mama mzazi katika malezi na makuzi ya mtoto. Katika makala haya kukosekana kwa mama kutajadiliwa katika nyanja mbili: kufariki na kutelekeza majukumu ya malezi kwa wazazi kutengana ama kutalikiana. Madhara yaliyojadiliwa katika sehemu hii ni changamoto za makuzi, simanzi na kukosa mwongozo wakati wa ukuaji.

**4.2.1 Changamoto katika ukuaji**

TUKI (2019) wamefasili neno changamoto katika fasili mbili. Fasili ya kwanza inafafanua changamoto kama kitu, hali au ambo linalotia hali ama pia hamu ya kufana kitu. Fasili ya pili inafafanua changamoto kama hali au jambo linalomweka mtu katika njia panda. Fasili hii ya pili ndiyo itatumika katika muktadha wa makala haya. Ni dhahiri kwamba kukosekana kwa wazazi katika malezi ya mtoto husababisha changamoto nyingi sana katika ukuaji wake. Chavda na Nisarga (2023) wanaeleza kwamba utoro ama kifo cha mzazi na migogoro baina ya wazazi waliotengana ama kutalikiana hakuathiri tu akili ya mtoto bali pia huathiri afya yake ya mwili, ukuaji na uhusiano na watu kwa siku zijazo. Hii ina maana kwamba mama anapokosekana katika ukuaji wa mtoto athari tajwa zinaweza kutokea kwa mtoto kwa kiasi kikubwa mno katika makuzi yake na hata ukubwani. Nyimbo za Bongo fleva zimesawiri madhara ya kukosekana kwa nafasi

ya mama katika malezi ya mtoto. Mwanamuziki B2K katika wimbo wake uitwao Mama anadhihirisha hilo anaposema

*Hukusema hata neno la mwisho mama wee*

*Kwa wengine ni furaha ila kwangu ni kilio*

*Ukuaji wangu changamoto haikuwa rahisi aisee*

*…nikwambie ya dunia yanaumiza sana*

*Nikwambie baba aliondoka mama*

Mishororo hii inadhihirisha namna watoto hupata changamoto katika ukuaji pale wanapofiwa na wazazi hasa mama. Mtunzi anasimulia kuhusu ukuaji wake ulivyokuwa na changamoto kutokana na kutokuwepo mama yake. Pia anaeleza namna anavyohuzunika kumkosa mama yake katika ukuaji wake. Ni dhahiri kwamba mwanamke ni mtu wa muhimu sana katika malezi ya watoto ndiyo maana mwanamuziki anaimba kwa wengine ni furaha ila kwake ni kilio kufiwa na mama yake na kukosekana katika malezi. Vilevile, mtunzi anasema ya dunia yanaumiza sana, huo ni mwendelezo wa kuonesha kwamba alipitia changamoto zilizomuumiza mno kutokana na kumkosa mama yake. Kwa kusema hivi ni dhahiri kwamba nafasi ya mwanamke katika malezi ni ya muhimu sana. Halikadhalika mwanamuziki K-Sal pia katika wimbo wake uitwao Mkiwa anathibitisha hilo anaposema

*Kuishi bila wazazi maisha yangu maigizo kwani sina mwongozo*

*Ndugu wa ukoo wangu kuishi nao kwa mzozo*

*Kula na kulala kwangu kwa shida na mizevezo*

*Ona haka ka mchezo*

*Nyumba ya pili imeibiwa naambiwa ni mimi*

*Huku mjini hakuna shamba naambiwa silimi*

*Uonevu kwangu hauishi vibao mpaka makonzi*

*… mlo wa usiku tu naupata kwenye njozi*

Mishororo hii inaonesha changamoto wanazopitia watoto waliofiwa na wazazi wao, mama akiwa ni mzazi pia. Sauti ya mtoto anayelalamika katika wimbo huu inaonesha changamoto anazopitia baada ya kuondokewa na wazazi wake akiwemo mwanamke ambaye ni mama, changamoto hizo ni mizozo ya mara kwa mara baina yake na ndugu wanaomlea, kula na kulala kwa shida, kupigwa na manyanyaso mengine. Changamoto nyingine ni kusingiziwa wizi hata katika nyumba za majirani ambazo huenda hana hata mazoea ya kufika huo. Pengine mama yake angekuwa hai yasingemfika hayo yote.

#### 4.2.2 Huzuni

Huzuni ni hali ya kuwa na masikitiko au majonzi. Ni dhahiri kwamba mwanamke anapokosekana katika malezi ya mtoto basi mtoto hukua kwa huzuni na simanzi sana, hii ni kwa sababu watoto husikia wenzao na rafiki zao wakisimulia mambo mazuri kuhusu mama zao. Wanaokosa malezi ya mama zao hubaki na huzuni kutokana na kukosa mama pembeni mwao. Katika sehemu ya 4.1 nafasi ya mwanamke katika malezi imejadiliwa kwa kina. Mambo yaliyotajwa katika sehemu hiyo yanapokosekana huleta huzuni kwa mtoto. Hili linadhihirika katika wimbo unaoitwa Mama ulioimbwa na mwanamuziki Bashary anaposema

*Sikia mama nakuuliza kwani nini mi nimefanya*

*Kama ugomvi we na daddy mimi yanihusu nini*

*Haukutaka kunilea mimi na ndiyo maana ukanitupa mammy*

Mishororo hiyo inasadifu huzuni aliyonayo mtoto katika wimbo huo. Anamlaumu mama yake kwa kumtelekeza na kuacha kumlea kwa sababu ya ugomvi kati yake na baba yake. Mara nyingi kunakuwa na changamoto za malezi pindi wazazi wanapokuwa na migogoro ama kutengana ama pia kutalikiana na wanaoathirika huwa ni watoto. Ni vyema pande zote kutumia busara na kuhakikisha kila mzazi anahusika katika malezi ili kudumisha furaha ya watoto na ukuaji mwema. Pia mwanamuziki Rayvanny katika wimbo uitwao Mama anasema

*Uko wapi mama rudi nikuone nateseka sana*

*Uko wapi mama mwanao nakumiss pumzika salama*

Mishororo hii inaonesha huzuni kutokuwepo kwa mama. Sauti katika wimbo huu inadhihirisha huzuni aliyonayo mtoto huyo kwa kumpoteza mama yake. Pia anazungumzia kumkumbuka mama yake, hii inadhihirisha kwamba nafasi ya mwanamke kama mama ni ya muhimu katika malezi na makuzi hata katika maisha ya baadaye. Fauka ya hayo mwanamuziki Afande Sele katika wimbo uitwao Mkuki Moyoni anasema

*Sasa baada ya kifo cha baba mama alisonga mbele kivyake*

*Miaka mingi ikapita sikupata salamu zake*

*Kwenye vyombo vya habari nikatuma ujumbe wake*

*Tena kuna gazeti lilitoa hadi picha zake*

*Waungwana walioziona walisema yuko Kigoma*

*Na zaidi wakanieleza kuhusu maisha yuko njema*

*Nikaenda kumtazama nipate kuhakikisha kama alipo ni salama*

*Unajua uchungu wa mama hasa mkipotezana kwa muda usiojulikana*

*Kwa bahati njema nikampata bahati mbaya ikafuata najuta yaliyonikuta…*

*Mama alinikataa kwanza sikumwelewa nikabaki namshangaa*

*Kisha nikamuuliza vipi mama una kichaa?*

*Mwenyewe umenizaa hivi sasa unanikataa?!*

*Jibu alilorudisha sikuamini kwa masaa*

*Alisema sikujui na geti akafunga paa!...*

*Kweli nilishangaa mama yangu alonizaa kuniacha kwenye mataa*

*Takribani nusu saa sikuongea kama bubu*

*Watu walinizunguka niliinama chini kwa aibu*

*Ntaishi vipi ugenini akilini sikuwa na jibu*

Mishororo hii inadhihirisha huzuni anayokuwa nayo mtoto kwa kutokuwepo mama yake katika malezi baada ya kupotezana kwa muda mrefu na anaamua kumtafuta. Huzuni yake inazidi pale mama yake anapomkana mbele za watu kwamba hamtambui na hajawahi kuzaa. Hii ni athari hasi ya kukosekana nafasi ya mama katika makuzi ya mtoto.

### 4.2.3 Kukosa mwongozo

Tafiti nyingi kuhusu malezi zinadai kwamba mama ndiye nguzo ya malezi katika familia. Zipo methali kadhaa pia zinazothibitisha dai hili kama jinsi falsafa ya kiafrika inavyoshadidia, mathalani *asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.* Methali hii hufafanuliwa katika maana mbalimbali lakini katika utafiti huu itafafanuliwa kwamba mama ndiye nguzo muhimu katika kuwafunza watoto mambo ya msingi katika maisha ikiwemo kufunza mambo mema na kuwaepusha na maovu. Ni dhahiri kwamba mwongozo wa mama ni wa muhimu sana katika malezi na makuzi ya watoto na inapotokea mama akawa hayupo basi watoto hukosa mwongozo hata katika maisha yao ya ukubwani. Hili linadhihirishwa na mwanamuziki Kasi Simela katika wimbo uitao Mama anaposema

*Nawe ndiyo taa yangu nyumbani nimebaki giza*

*Nikiona picha yako inabaki kuniliza liza*

Mishororo hii inadhihirisha kwamba mama anapokosekana katika maisha ya watoto hukosa mwongozo sahihi kutokana na uzoefu wa matukio waliyopitia. Mwongozo huo ndiyo humwelekeza mtoto katika kutofautisha mema na mabaya katika maisha yake na hata upendo na mambo mengine mengi. Hili linaungwa mkono na mwanamuziki K-Sal kwatika wimbo uitwao Mkiwa anaposema

*Kuishi bila wazazi maisha yangu maigizo kwani sina mwongozo*

Mshororo huu unathibitisha kwamba wazazi ni watu wa muhimu katika kutoa mwongozo katika ukuaji wa watoto akiwemo mwanamke pia hili husababishwa na baadhi ya walezi kutowapa mwongozo wowote watoto hao wanaowalea. Mwanamuziki anayafananisha maisha yake na maigizo ambayo kimsingi si uhalisia wa maisha isipokuwa ni mwigo tu wa matendo na tabia katika maisha. Kwa mantiki ya makala haya ni kwamba mwanamke kama mzazi anapokosekana

katika maisha ya mtoto huyafanya maisha yake kuwa magumu na pengine kukosa maana halisi kipindi cha ukuaji.

## 5.0 Hitimisho

Makala haya yamejadili nafasi ya mwanamke katika malezi kwenye jamii kama alivyosawiriwa katika nyimbo teule za Bongo fleva. Utafiti umebaini umuhimu wa mwanamke katika makuzi ya mtoto na malezi kwa ujumla. Aidha utafiti umefafanua madhara ya kukosekana mwanamke katika malezi ya watoto ambayo yamejdiliwa kwa kuonesha namna yanavyoweza kuathiri ukuaji wa mtoto na maendeleo yake ya baadaye. Ni dhahiri kwamba mwanamke ana nafasi kubwa na yenye kuheshimika katika malezi kwenye jamii. Pamoja na kwamba uhusika wa mwanamke katika malezi haupewi heshima katika jamii kwa kuchukuliwa kama jukumu la asili la mwanamke, jambo hili ndilo muhimu sana katika ukuaji wa kila mtu.

## 6.0 Mapendekezo

Utafiti unapendekeza wazazi wote kuhusika katika makuzi ya watoto bila kujali tofauti zozote lakini pia walezi ambao wanalea watoto baada ya kufiwa na wazazi wawalee kwa upendo hata wasijihisi kuna vitu wanakosa katika ukuaji wao.

## Marejeleo


Allen, G. (2000). *Intertexuality.* Routledge.

Chavda, K., & Nisarga, V. (2023). Single parenting: Impact on child's development. *Journal of Indian Association for Child and Adoloscent Mental Health,* 1(19), 14-20.

Kasiga, G. A. (2021). Athari za U-Nigeria katika video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania. *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences (RUJASS),* 7(1), 118-135.

Kohrs-Amissah, E. (2002). *Aspect of feminism and gender in the novels of three West African women writers (Aidoo, Emecheta, Darko).* Books on African Studies.

Kristeva, J. (1980). *Desire in language: A semiotic approach to literature and art.* (kimetafsiriwa katika Kiingerza na L. S. Roudiez, T. Gora, A. Jardine, & L. S. Roudiez). Columbia University Press.

Kyarendwa, F. K. (2014). *Usemezano katika riwaya ya kiswahili.* Tasnifu ya Umahiri. (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Lucas, C. B. (2022). Usawiri wa taswira za ngono katika nyimbo za bongo fleva: Mifano kutoka nyimbo teule za WCB. *Jarida la CHALUFAKITA,* 4, 65-79.

Lupogo, I. (2019). "Sababu za kuibuka, kung'ara, na kupotea kwa wasanii katika tasnia ya muziki wa bongo fleva: Uchunguzi wa kategoria maalumu ya nyimbo hizo". *MULIKA,* 38, 126-140.

Chama Cha Mapinduzi. (1987). *Sera ya taifa ya malezi kwa watoto na vijana Tanzania.* Chama Cha Mapinduzi.

Mwananchi. (2018, Novemba 18). *Fahamu maana halisi ya malezi na ulinzi wamtoto.*Imesomwa Mei 4, 2024, kutoka https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/makala/johari/fahamu-maana-halisi-ya-malezi-na-ulinzi-wa-mtoto-wako-2940244

Al-Azhar Observatory. (2021, Julai 18). *Mpango wa malezi bora katika kupambana na fikra kali.* Ilisomwa Mei 4, 2023, kutoka tovuti ya Kituo cha Uangalizi cha Al-Azhar: https://www.azhar.eg/observer-swahili/DetailsSwahili/ArtMID/2216/ArticleID/55623/Mchango-wa-Malezi-Bora-katika-Kupambana-na-Fikra-Kali

Omari, S. (2009). *Tanzania Hip Hop poetry as popular literature.* Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Samwel, M. (2015). *Umahiri katika fasihi ya kiswahili: Mwongozo kwa mwanafunzi na mwalimu wa fasihi simulizi na andishi.* MVP.

Steady, F. C. (1981). *The black women cross-culturally.* Schenkman Publishing Company.

Sema Tanzania. (2023, Agosti 13). *Namna sita mzazi anavyoweza kuhakikisha malezi bora kwa mtoto.* Ilisomwa Mei 4, 2024, kutoka The Chanzo Initiative: https://www.thechanzo.com/2023/08/13/namna-sita-mzazi-anavyoweza-kuhakikisha-mlezi-bora-kwa-mtoto

TUKI. (2019). *Kamusi ya kiswahili sanifu.* Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya fasihi istilahi na nadharia.* East African Educational Publishers.

Wamitila, W. (2008). *Kazi ya fasihi: Misingi na uchanganuzi wa fasihi.* Daisy Printers (K) Limited.